

**MUNGU ANADHIHIRISHWA
KUPITIA KWA YESU KRISTO.**

**MUHTASARI WA UTANGULIZI WA THIOLOGIA YA
USHIRIKA WA NAFSI TATU ZA UUNGU.**



**GRACE
COMMUNION
INTERNATIONAL
*LIVING AND SHARING THE GOSPEL***

MUNGU ANADHIHIRISHWA NA YESU KRISTO.

MUHTASARI WA UTANGULIZI WA THIOLOGIA YA

USHIRIKA WA NAFSI TATU ZA UUNGU.

Yeyote atakaye kupata picha halis ya Mungu, picha hiyo haiwezi kupatikana bila kumwagalia Yesu Kristo. Ndani ya Yesu tunamuona Mungu dhahiri kama alivyo.

Yesu katika kitabu cha Yohana mtakatifu 14:9 anasema “Mimi nimekuwepo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemuona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?”

Maandiko yote yatanukuliwa kutoka The Holy Bible in Kiswahili Union Version Iliyochapishwa na Bible society of Tanzania.

Yesu Kristo ndiye ufunuo halisi wa Mungu Baba. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua. (Yohana 1:18)

Kitabu hiki kinapatikana kwa lugha ya kiingereza na pia kwa wanaoishi katika nchi ya Marekani unaweza kuagiza katika tofuti ya kanisa <http://www.gci.org/participate/request>

Kwa maneno ya Yesu na kwa matendo yake, tunasikia na kuona mambo ambayo ni ya msingi kwa kila binadamu – kuwa upendo wa Mungu kwa wanadamu hauna mipaka. Alimtuma Yesu kutokana na upendo huu na uimara wa nia yake ya ukombozi wa mwanadamu. Unapomjua Yesu unamjua Mungu, ikimaanisha kuwa tunayoyaamini kuhusu Yesu ndo msimamo wetu wa kithiologia.

Kwa njia moja ama nyingine, kila mmoja wetu anayo thiologia. Kwa kifupi thiologia ni “Ufahamu au uelewa kuhusu Mungu”. Kwa kifupi tunaloamini kuwa ukweli kuhusu Mungu ndio thiolojia yetu.

Hakika kila kanisa na hata ndini inaomwongozo wa thiolojia. Ni misingi ambayo inawaonyesha na kuwaeleza msimamo wao wa kidini na pia matendo yao ya Kikristo.

Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu inatazama ushirika huo kama kiini na msingi wa kuisoma Biblia, pia thiolojia inapaswa kuelezwa kutokana na misingi hii.

Thiolojia hii haijijhusishi tu na jinsi, kwa nini au matendo lakini ya maana zaidi thiolojia hii inaanza kwa kutazama “Yupi”, thiolojia hii inaanza kwa kuuliza jinsi Mungu anavyowakilishwa na Yesu Kristo, na pili sisi tunayo nafasi gani katika ushirika huu?

Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu hairejelei kijujuu imani ya mafunzo ya ushirika wa nafsi tatu (mafunzo ya Biblia kuwa yupo Mungu mmoja aishiye milele kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu) bali inarejelea Yesu Kristo kama chanzo cha kuelewa Mungu ni nani.

YESU KRISTO KAMA KIINI:

Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu kimsingi inamtazama Yesu Kristo kama kiini – kama inavyoelezwa na mwana thiologia anaye sifika kama mwalimu wa Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu katika karne ya ishirini Thomas F. Torrance, Yesu Kristo anadhihirika kama neno la Mungu kwa mwanadamu na vile vile anadhihirika kama neno la mwanadamu kwa Mungu. Kwa sababu hii, hata maandiko matakatifu yako chini ya utawala wake.

Yesu Kristo kwa wakati mmoja alieleza kuwa yeye ndiye mwanzo wa kuyaelewa maandiko. Aliwaambia viongozi wa kidini wakati huo “Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima”. (Yohana 5:39-40).

Tunapenda kuisoma na kuitafsiri Biblia kwa mtazamo wa Yesu Kristo. Ndiye msingi na njia ya kweli ya thiolojia inayofaa. Kwa kuwa yeye pekee ndiye mwanzo na mwisho wa ufunuo wa wazi wa Mungu kwetu wanadamu.

KIINI CHA UHUSIANO:

Kwa kuwa Yesu Kristo ndiye kiini, basi thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu msingi wake ni katika uhusiano. Yesu Kristo ambaye ndiye mwana wa pekee wa Mungu Baba, ameunganika na nafsi zetu na kutokana na muungano huu akafanyika kafara na ondoleo la dhambi zetu, kwa hali hiyo anatuwakilisha kama ndugu na dada kwa Mungu Baba. (Yohana 1: 14; Waefeso 1:9-10; 20-23).

Kwa sababu ya Kristo, tunao uhusiano na Mungu! Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu. Sisi tumefanywa wana wa Mungu na vile vile tuko ndani ya Kristo, ambaye ni kipenzi chake Mungu Baba.

Kwa muhtasari uhusiano huu kwa wanaomwamini Kristo unamaanisha mambo manne kwa maisha na imani yao:

1. Uhusiano wa kiundani, wa milele na wa upendo wanaoshirikisha Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

2. Uhusiano wa unganiko na wa milele wanaoshirikisha Mwana na wanadamu ndani ya Yesu Kristo aliyebadilishwa na kuchukua mwili wa binadamu.
3. Uhusiano wa wanadamu na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.
4. Uhusiano wa wanadamu na wenzano kama watoto wa Mungu waliokombolewa kwa damu ya Yesu Kristo.

HISTORIA YA THIOLOJIA YA USHIRIKA WA NAFSI TATU ZA UUNGU

Katika karne ya Ishirini, Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ilienea katika nchi za magharibi kupitia kwa mwanathiolojia Karl Barth na wanafunzi wake hasa Thomas F. Torrance na ndugu yake James B. Torrance.

Lakini thiolojia hii inayo miaka mingi kama kanisa lilivyo na miaka mingi. Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ndiyo iliyokuwa misingi ya mafundisho ya kwanza kwa wakiristo. Hii inadhahirika katika tamko la fumbo la imani ya mitume, tamko la fumbo la imani ya Nicene na pia kwenye ufafanuzi uliojulikana na Chalcedon. Wanathiolojia mashuhuri na waalimu wa mwanzo wa Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ni kama vile; Irenaeus, Athanasius, na Gregory wa Nazianzus.

Irenaeus (aliyefariki mwaka wa 202 baada ya kuzaliwa kwa Kristo) alikuwa mwenyeji wa mji wa Polycarp (alikuwa wanafunzi pamoja na Mtume Yohana) Irenaeus alitoa ufafanuzi kuwa injili ya ukombozi kama ilivyofundishwa na mitume na kuendelezwa na wengine baada yao ilinua kueleza Kristo kama kiini cha wokovu na uhusiano wetu na Mungu. Aliiona Biblia kama inayoeleza badiliko la Yesu kufanywa kama binadamu ili kutoa mwanzo mpya kwa wanadamu.

Kupitia kwa badiliko la Yesu kufanywa kama binadamu, wanadamu kwa ujumla wao “wamezaliwa upya” katika Yesu Kristo, wamekombolewa kutoka kwa dhambi na mauti ambayo imemfanya mwanadamu mtumwa tangu enzi za Adamu. Kupitia kwa Yesu Kristo, wanadamu wamepeleleka mwanzo mpya na wanatambulika tofauti na walivyojulikana.

Misingi ya kibiblia ya wanathiolojia Irenaeus’ uliuhusisha tamko la Mtume Paulo katika kitabu cha Warumi 5 ambapo Mtume Paulo anamwakilisha Yesu kama Adamu wa pili na wa mwisho kwa wanadamu. Aliandika Irenaeus’, “katika Yesu Mungu alijigeuza na kujifanananisha na mwanadamu wa kwanza (Adamu) akiwa na nia ya kuangamiza dhambi, kuipokonya maiti nguvu zake na kutakasa mwanadamu....” (Nukuliwa Heresies, III.18.7).

Irenaeus alielewa kuwa Yesu alijitwika ubinadamu wetu wote akiwa kama mwakilishi mbele zake Mungu na vile vile kama kafara inayostahili mbele zake Mungu, kwa kitendo

hicho akayafanya upya maisha ya mwanadamu kupitia kwa uhai wake, kifo chake na kufuliwa kwake.

Irenaeus alifundisha kuwa kufanywa upya au kuubwa upya kwa wanadamu, kupitia kwa Yesu Kristo sio kitendo tu kilichofanywa na Yesu, sio tu msamaha wa dhambi zetu bali ukombozi wetu kwa ujumla wake unahusu kuumbwa upya ndani na kupitia kwa Yesu Kristo.

Athanasius (aliyefariki mwaka wa 373 baada ya kuzaliwa kwa Kristo) alitetea injili kutoka kwa walimu wa uongo ambao hawakuamini umilele na Uungu wa Mwana (Yesu Kristo). Msimamo wake ndio uliophelekea kubuniwa kwa mafunzo ya kidini ya Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ambayo ilidhimbitishwa katika kikao cha Nicea cha mwaka 325 baada ya kifo cha Kiristo. Katika kutetea kwake Athanasius alisema yafuatayo:

Kwa hali hiyo, kwa kuchukua mwili kama tulionao, na kwa kuwa mili yetu imehukumiwa kifo, ilijinyenyekeza hadi kifo kwa niamba yetu wote, na kafara hii aliitoa kwa Baba. Haya aliyetanda kutokana na upendo wa pekee kwetu ili kwa maiti yake wote tunakufa..... Hili alilitenda ili kuwageuza wanadamu waliopotea na kuwafanya upya kupitia kwa mauti kwa kulipa kwa mwili na neema za kufufuliwa kwake (sehemu ya 8).

Kwa kafara hii, Mungu angefanya lingine lipi? Akiwa Mungu alipata nafasi ya kuifufua sura yake kwa wanadamu, ili kupitia kwa kafara hiyo wanadamu wangemjua upya. Hili lingefanyika kwa njia nyingine ipi tofauti na Mungu kujileta kupitia kwa Mwanaye Yesu Kristo?.

Neno la Mungu lilikuja kupitia kwake mwenyewe kwa kuwa ni yeye pekee mwakilishi wa Mungu Baba, aliyekuwa na uwezo wa kuumba upya mwanadamu aliyeumbwa kwa sura yake. Kwa hali hiyo matendo makuu mawili yalifanyika kwa wakati mmoja, kifo cha wote wanaomwamini na kuenzi mwili wa Yesu, na kwa kuwa neno lilikuwa ndani yake, mauti na dhambi kwa wakati huo huo zikaangamizwa. kuwepo kwa hukumu ya mauti kutokana na dhambi iliharalisha kuwepo kwa dhambihu la ondoleo la hukumu hiyo (Sehemu ya 13).

Kwa kuwa neno (Yesu) asingeweza kufa, ililazimu kujitwika mwili wa mauti ambao angeutoa kama kafara kwa ajili ya wote, akaumizwa kwa ajili ya wote. Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilishi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. (Waebrania 2:14-15) (Sehemu ya 20)

Kwa kupitia kwa kifo chake, wanadamu wote wamekombolewa, viumbe wote wamepate urejesho. (Sehemu 37).

Athanasius na Irenaeus walisisitiza kuwa kubandilishwa kwa Mwana kuchukua umbo la mwanadamu, tukio hili lilihusu kila mwanadamu. Mungu aliamua kumuokoa mwanadamu kupitia kwa kuzaliwa, maisha, kifo cha kafara na kufufuliwa kwa Mwana wa Mungu. Huu ndio msingi wa Injili kama walivyoielewa wakristo wa kwanza na inavyofunuliwa katika maandiko.

Gregory wa Nazianzus (aliyefariki mwaka wa 389 baada ya kuzaliwa kwa Kristo) aliandika jinsi Kristo alivyoshiriki katika urejesho baada ya kuvunjika kwa uhusiano wetu kupitia kwa kuvaa mwili wa mwanadamu:

Kwa kuwa aliuchukua mwili wa binadamu, basi hiyo ilileta uponyaji kwa miili yetu. Alichounganisha na Mungu kimeokolewa. Kama Adamu angeanguka nusu basi alichookoa Yesu kingekuwa nusu, lakini kama kweli wanadamu walianguka kwa ujumla, basi walipaswa kuunganishwa kiujumla na nafsi ambayo ilikuwa binadamu kwa ujumla ili ukombozi uje kwa binadamu kikamilifu. (Epistle 101)

Katika kuuchukua mwili wa binadamu, Kristo alijiunganisha na hali tuliyokuwa nayo, kwa kifupi na mwanadamu aliyekuwa ameanguka dhambini, ili kumrejesho. Kama alivyopenda kusema J.B. Torrance daktari akageuka kuwa mgonjwa ili kuleta uponyaji. Ni muhimu kujua kuwa Mungu kupitia kwa Kristo anatupenda kiasi cha kutukumbatia hata wakati tulipokuwa dhambini.

WEWE NI NANI, BWANA?

Wewe ni nani, Bwana? Mtume Paulo alihangaika na swali hili katika njia ya kwenda Dameski, ambapo alikutana na Kristo aliyefufuliwa. (Matendo ya Mitume 9:5). Baada ya tukio hili, Mtume Paulo alitumia miaka yake yote akijibu swali hilo. Alieleza kwa wote ambao wangemsikiliza jibu la swali “Wewe ni nani, Bwana?” Jibu ambalo linaelezwa katika maandiko, ndio msingi na kiini cha thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu.

Yesu kikamilifu ni Mungu na kikamilifu ni mwanadamu na milele itakuwa hivyo. Kubadilishwa kuuchukua mwili wa binadamu haikuisha wakati wa kifo na kuinuliwa kwake. Itaendelea kuwa hivyo milele yote. Alifufuka na kuinuliwa akiwa na mwili na katika kurejea kwake atarejea kama alivyoinuliwa. Kwa hivyo tunapongea habari za Yesu Kristo tunaongea kuhusu Mungu na vile vile mwanadamu.

Kama aliye Mungu, (Muumba na mhifadhi wa vyote) na wakati huo huo akiwa kama binadamu kikamilifu, hali hii inamuweka katika nafasi ya pekee katika ushirika wake na Mungu na pia katika ushirika wake na wanadamu. Katika na kupitia kwa maisha, kifo,

kufufuka na kuinuliwa binguni kwake, wanadamu wote wanashirikishwa katika maisha na upendo wa Mungu. Kama mtume Paulo alivyoandika; “Kwasababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; (hii inaongelea wakati uliopita, wakati huu na wakati ujao)- (1 Timotheo 2:5).

KRISTO KWA AJILI YA WOTE.

Upana wa maisha ya kushangaza ya Kristo unakumbatia wanadamu wote waliowahi kuishi, wanaoishi na watakaoishi.

Kwa hali hii Biblia inasema wazi Kristo alikufa kwa ajili ya wanadamu wote. Mafungu ya Biblia yanayoeleza haya ni kama ifuatavyo:

- Yohana 12:32: “Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu”.
- 2 Wakorintho 5:14: “Maana, upendo wa Kristo watubisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote;”
- Wakolosai 1:19-20: “Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.”
- 1 Timotheo 2:3-6: “Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake.”
- 1 Timotheo 4:9-10: “Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa; kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio.”
- Waebrania 2:9: “Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.”
- 1 Yohana 2:2: “naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwangu wote.”
- Pia tazama Yohana 1:29; 3:17; Warumi 8:32; 2 Wakorintho 5:18-19; Tito 2:11; na 1 Yohana 4:14.

Mafungu haya yanaiweka wazi kuwa kifo cha Yesu kilikuwa kafara kwa ajili ya ondoleo la dhambi za kila mwanadamu.

YESU, ADAMU WA PILI.

Katika kitabu cha warumi 5, Mtume Paulo aliwahutumbia Warumi lakini alilowaambia linahusu wanadamu wote wanaoamini na wasioamini. Kulingana na Mtume Paulo, kupitia kwa Yesu Kristo, kila mwanadamu:-

- Ameharalishwa kupitia kwa imani katika Yesu Kristo (fungu. 1, 18).
- Amepata amani kwa Mungu (fungu. 1).
- Ameifikia neema ambayo anasimama ndani yake. (fungu. 2).
- Amepatanishwa na Mungu kupitia kwa mauti ya Yesu (fungu. 10).
- Ameokolewa kupitia uzima wake Yesu Kristo. (fungu. 10).

Kuharalishwa, kupatanishwa na kuokolewa kulitokea wakati:

- “Tulipokuwa hatuna nguvu” (fungu. 6).
- “Tulipokuwa tungali wenye dhambi” (fungu. 8).
- “Tukiwa bado adui za Mungu” (v. 10).

Mungu alitenda haya yote kwa ajili yetu hata kabla hatujazaliwa. Faida ya tendo la Kristo lililofanyika miaka mingi iliyopita zinamaana kwa wakati uliopita, uliopo na hata wakati ujao. Mtume Paulo anasema “zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake”. (fungu. 10)— hii ikidhihirisha kuwa wokovu sio tukio la mara moja mbali ni uhusiano endelevu kati ya Mungu na wanadamu – uhusiano uliobuniwa ndani na kupitia kwa Yesu Kristo ambaye kupitia kwake amewapatanisha wanadamu na Mungu kwa amani.

Tukiendelea na Warumi 5, Mtume Paulo anaoanisha Adamu na Yesu huku akimwita Yesu Adamu wa pili na wa mwisho. Tambua maelezo ya msingi ya Mtume Paulo ni:

- “.... Kama kwa mtu mmoja (Adamu) dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti...” (fungu. 12).
- “..... zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake mwanadamu mmoja Yesu Kristo (Adamu wa pili) kimezidi kwa ajili ya wale wengi. (fungu. 15).
- Basi tena, kama kosa moja watu wote walihukumiwa adhambu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. (fungu. 18).

Sio kwamba Yesu kwa ujumla ametutendea tendo njema tu mbali ametushirikisha katika kulitenda jambo hilo njema, ametushirikisha katika maisha yake, kifo chake, kufufuliwa kwake na kupandishwa kwake mbinguni.

Kwa hali hiyo, mafungu Biblia inatueleza kuwa:

- Alipokufa Yesu wanadamu wote walikufa pamoja naye.
- Alipofufuka Yesu wanadamu wote walifufuliwa katika maisha mapya ndani yake na pamoja naye.
- Alipopandishwa, wanadamu wote tulipandishwa na tukaketishwa pamoja naye katika mkono wa kuume wa Mungu Baba. (Waefeso 2:4-6).

Wanadamu wanapoamini, wanaanza kumfahamu Yesu na kushiriki katika uhusiano pamoja naye.

WOKOVU NI KUUMBWA UPYA.

Mujiza wa kubandilishwa Yesu Kristo kuvikwa mwili wa kibibadamu sio tukio lililofanyika “miaka mingi iliyopita”. Tukio hili lilibadilisha mfumo wa ulimwengu na kuufanya kiumbe kipya (2 Wakorintho 5:17). Mabadiliko haya yalibadilisha mfumo wa ulimwengu milele, ikirudi nyuma kuwafikia wanadamu wa nyuma na vile vile ikifunguka kuwakumbatia wanadamu wa maisha yote ya baadaye.

Mtume Paulo akiongea kuhusu badiliko hili katika Waraka kwa Warumi 7:4 ambapo anasema, hata wakati tuko hai bali tunakuwa wafu kwa sheria kupitia kwa mwili wa Yesu Kristo. Kifo cha Yesu akiwa mwanadamu kwa ajili yetu katika tukio la kihistoria ni dhihirisho la kisasa linalohusisha wanadamu wote (wazamani, wasasa na watakapo kuja). Mtume Paulo akawaandikia Wakolosai: “Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu” (Wakolosai 3:3). Hata kabla hatujafa kifo cha kawaida, kwa sasa tumekufa katika kifo cha Kristo na katika kufufuka kwake tumefanywa kuwa hai.

Unganiko letu katika maisha, kifo, ufufuo na kupandishwa kwa Yesu Kristo inaelewa vyema katika Waraka kwa Waefeso 2:5-6 Mtume Paulo katika waraka huu anaeleza kuwa kama ambavyo tumekufa katika kifo cha Yesu, tumeshafufuliwa pamoja naye na tumepandishwa pamoja naye, tukiketishwa pamoja naye katika ufalme wa mbinguni, haya yote yanatokana na neema za Mungu.

Ushirika wa Mungu na wanadamu kupitia kwa Yesu unashirikisha wanadamu wote hata wale walioishi kabla ya kuja kwa Yesu duniani.

IMANI KATIKA YESU:

Inamaanisha nini kuokolewa kwa neema kupitia kwa imani? Ina maana tunaokolewa kwa jambo tulilotenda, tendo la kibinadamu au la imani? Kama ni hivyo, basi nini kitakachotokea kwetu wakati imani yetu inafifia au hatuna imani kabisa? Habari njema ni kuwa Yesu ameshafanya yote yaliyopaswa kwa ajili ya wokovu wetu kutoka mwanzo mpaka mwisho, hata kuamini kwa niamba yetu. Mwana thiolojia David Torrance aliandika:

Tunaokolewa kwa imani ya Yesu, na utii wake kwa Mungu Baba sio kwa imani yetu wala utii wetu. Ndugu yangu Tom (Torrance) alipenda kunukuu Wagalatia 2:20 “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Haya ndiyo maandiko kwenye Biblia na ninaamini imetafsiriwa vizuri kutoka kwa Kigiriki.....

Tafsiri zingine kama vile New International Version, waliipata vigumu kuamini kuwa tunaweza kuishi kupitia kwa imani ya Kristo mbali na imani yetu, kwa hivyo wakabadilisha tafsiri ili isomeke: “Ninaishi kwa imani ndani ya Mwana wa Mungu”- Hii ina maana tofauti kabisa na maandiko ya mwanzo. Tafsiri hii inaondoa maana halisi ya maisha ya kushangaza ya imani ya Yesu. Ni kupitia kwa imani yake Yesu (sio yetu) ndio tunaokolewa na tunaishi, imani yetu ni ishara tu ya shukrani kwake kwa ajili ya imani yake.

Tunapogeuka nyuma na kuona na kutafakari jinsi tulivyokuwa na tunavyoendelea kutotii, inatia moyo mno tukikumbuka na kujua kuwa Yesu ametoa maisha yake kamilifu kwa Mungu kwa ajili yetu, na ni utii wake Yesu unaohesabiwa. Tunaokolewa kwa sababu ya utii wake, sio wetu. (Nukuu kutoka – Utangulizi wa Thiolojia na Torrance- Ukurasa 7-8).

KATIKA NAFASI YETU.

Biblia inaeleza wazi kwamba Yesu ndiye Alfa na Omega Mwanzo na mwisho (Ufunuo 22:13). Ndiyo maana tunaweza kuwa na imani kwake kuwa, ukamilifu wetu uko ndani yake bila hofu ya imani yetu kuwa nzuri au kutotosha. Mwana theolojia Thomas Torrance anaileza kama ifuatavyo:

Yesu anaingilia kati katika matukio tunapotakiwa kuonyesha imani yetu kwa Mungu, kuonyesha tumaini letu kwa Mungu na haki yetu mbele ya Mungu, Yesu huwa anasimama kwa ajili na kwa niaba yetu, huku akibadilisha kutoamini kwetu na imani yake ambayo tunashiriki. Kwa kifupi tunapofikiria imani, tumaini na haki kama matendo ya mwanadamu kwa Mungu, basi tunapaswa kumfikiria Yesu kama mwenye imani, tumaini na mwenye haki mbele za Mungu kwa niaba yetu.

Kupitia kwa kubandilishwa kwake na kuchukua mwili wa binadamu, kupitia upatanisho wa Yesu Krsito na wanadamu, imani yake imeoanishwa na imani yetu, kwa oanisho hilo badala ya kufinyiliwa kwa sababu ya ubinadamu wetu, badala ya kudhalilishwa, uoanisho hilo bila kusita linatutenganisha na ubinadamu wetu mbele zake Mungu. Imani yetu ikichukuliwa kama ilivyo, kama alivyosema mara kwa mara mwana Thiolojia Calvin, imani ni kama chombo ambacho hakijajazwa na chochote, kwa kuwa imani yetu inategemea uaminifu wa Yesu Kristo ili tupate pumziko na pia pumziko letu linategemea kustiliwa na uaminifu wake. (Nukuu kutoka kitabu cha Mediation of Christ, ukurasa. 82-84)

NA JE TUTASEMAJE KUHUSU MAAMUZI YA WANADAMU?

Kama ni maisha, imani na utii wa Yesu Kristo unaotuokoa na kutufanya sehemu ya wokovu, je wajibu wetu ni nini? Kabla ya kujadili wajibu wa mwanadamu, ni vema turejeele ukweli wa mafungu yafuatayo ya Biblia: Kupitia ushirika wetu na Yesu Kristo, wanadamu wote:-

- Wamepatanishwa na Mungu,
- Wamependwa na kukumbatiwa na Mungu,
- Wamekubalika katika pendo (Waefeso 1:6, KJV), na
- Wamesamehewa (hakuna kumbukumbu ya dhambi wala hukumu).

Injili haitangazi uwezekano wa haya mambo kuwa kweli katika maisha yetu, lakini ukweli ni kwamba wanadamu wanahimizwa kutoa ukumbali wao. Kupitia himizo la Roho Mtakatifu tunaweza kukumbali bila sharti kuukaribisha ukweli huu na kujiunga, lakini Mungu hatushurutishi kuukumbali. Mungu anasisitiza kuwa upendo lazima utolewe bure na upokelewe bure, hauwezi kushurutishwa bali utakuwa sio upendo.

Pamoja na kwamba uaminifu kwa uhuru tuliopewa na Mungu lazima uzingatiwe, lazima pia izingatiwe kuwa wanadamu walianzia uhusiano huu katika dhambi, (hawakustahili), kwa hali hii uwezo wa kuchagua kupenda au kutoupenda upendo wa Mungu ulikuwa umeisha. Kwa kuwa ukweli wa wanadamu umeoanisha na ukweli wa Yesu, basi kumkataa Mungu ingekuwa hatua ya uongo na kwa hatua hiyo tunarejeele tena utumwa. Ukweli na uhuru huwa zinaenda pamoja, kama tunavyokumbushwa mara kwa mara na mwanathiolojia Karl Barth:

Uhuru wa kweli wa mwanadamu unaamuliwa na ukweli kwamba Mungu ni Mungu wa mwanadamu. Katika uhuru huo, anao uamuzi mmoja tu wa kuchagua kuwa mtumishi wa Mungu, kwa kifupi kumimina shukrani zake kwa Mungu. Akiamua kuchagua lingine atakuwa tu kama kipofu akifuata njia asiojua, akiusaliti na kuuharibu ubinadamu wake.

Badala ya kuuchagua uhuru atakuwa akichagua utumwa. (Church Dogmatics IV.1, Kur. 43)

Kwa hiyo wajibu wetu ni nini? Tunapaswa kujitoa bila kushurutishwa kuwa waaminifu kwa injili, tukitoe shukrani zetu kwa mioyo iliyojaa tumaini, tukiinuana na kujengana mmoja kwa mwingine ndani ya mwili wa Yesu Kristo. Tunaposherehekea ukweli wa neema pamoja katika ushirika na ibaada zetu, maisha yetu hakika yatabadilishwa.

Wajibu wa kila mmoja:

Lazima tuchukue tahadhari tusije tukakanganya ukweli wa Yesu Kristo kwa wanadamu, na wajibu wa kila mtu anavyotakiwa kuwajibika kwa ukweli huu.

Hatumwamulii Yesu, kana kwamba maamuzi yetu ndiyo yanayoleta wokovu, bali tunakumbali tulichopewe ndani ya Kristo, tukiweka imani yetu kwa ambaye tayari ameshaweka imani yake kwa niamba yetu.

Tunapoiamini injili, ambayo ni ukumbali wa kulichogetu kwa neema, tunaanza kushiriki katika upendo wa Mungu kwetu. Tunaanza kuishi maisha ya kiumbe kipya ambacho Mungu hata kabla ya kuamini kwetu alitufanya ndani ya Kristo.

Upo ule ujumla au lengo la ukweli kwa wanadamu wote na pia kuna ukweli wa mtu binafsi ambao unamuongoza kumuelekeza kwenye maisha ya ukweli.

Kimalengo, kila binadamu waliopita, wanaoishi na watakaoishi, tayari wameharalishwa, wametakaswa, wote wamepata urejesho katika Kristo na kupitia alilolifanya kama mwakilishi wao na kwa kuchukua nafasi yao. Katika Yesu kimalengo tayari ni viumbe wapya, tukiwakilishwa kama viumbe wapya mbele ya Mungu na pamoja na Mungu.

Licha ya hayo, pamoja na kwamba wanadamu wamesharejeshwa na Yesu Kristo, sio wote wameitikia wito huo binafsi na kupata uamusho wa kuitikia na kukumbali alilolifanya Mungu kwa niamba yao. Hawajatambua kwa hakika nafasi waliopewa katika ushirika na Yesu Kristo.

Ukweli uliokusudiwa kwa wanadamu wote lazima upokelewe katika maisha binafsi ya kila binadamu na uwe sehemu ya maisha ya kila binadamu kwa kutubu na kwa imani. Kutubu na imani hazileti wokovu, lakini mwanadamu hawezi kufurahia wokovu bila ya kutubu na bila kuwa na imani. Ikumbukwe pia kutubu na imani ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Katika maandiko, tunapata mafungu yanayoongelea kuhusu lililokusudiwa kwa wokovu wa wanadamu kwa ujumla na pia mafungu yanaliyokusudiwa kwa wokovu wa

wanadamu kama binafsi. Yote ni ya kweli na hakika – lakini yale ya binafsi ni ya kweli kwa kuwa yale ya ujumla yalilenga maisha kabla ya kukumbali wito.

Mafungu ya ukweli uliokusudiwa kwa wokovu wa wanadamu kwa ujumla na mafungu yanaliyokusudiwa kwa wokovu wa wanadamu kama binafsi yanapatikana katika sehemu nyingi katika Biblia. Wakati mwingine yote mawili yakipatikana katika fungu moja katika Biblia.

Katika 2 Wakorintho 5:18-21 Mtume Paulo anaanza fungu la 18-19 kwa kusudi la jumla la wokovu, “Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.”

Hapo ni ukweli wa ujumla unaozingatia lililokusudiwa kwa wanadamu wote – kwamba wote wamerejeshwa kwa Mungu kupitia kwa tendo la Kristo kwa kuunganishwa na wanadamu wote.

Baada ya kudhibitisha ukweli wa wito wa jumla katika 2 Wakorintho 5:18-21, Mtume Paulo anaendelea katika fungu la 20-21 kueleza wito wa binafsi “Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anaishi kwa vinywa nyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye”.

Inawezekanaje kwamba wote tumepata urejesho na vile vile tunaalikwa ili turejeshwe? – ikionyesha kana kwamba urejesho haujatimia? Jibu ni kwamba yote mawili yako sawa – hizi ni pande mbili za ukweli kwamba wote kupitia kwa Yesu Kristo tumepata urejesho, huu ni urejesho wa jumla, lakini sio wote wamemkumbatia Kristo hivyo sio wote wanaoshiriki kwenye huo urejesho kwa Mungu.

Kurejeshwa na mtu asijue na asishiriki ataendelea kuishi kana kwamba hajarejeshwa . kufunuliwa macho na Roho Mtakatifu mtu apate kuuona urejesho, aamue kuukumbatia na kushiriki hakufanyi urejesho kufanyika, bali huumbandilisha urejesho kuwa binafsi na ushirika wake na Mungu kuwa binafsi.

Kwa hiyo, wito wa kiinjilisti kuwa wajumbe kwa ajili ya Kristo (fungu 20) unamaanisha turejeshwe. Lakini wito huu sio tufanye kitu ili tusababishe Mungu aturejeshwe kwake; bali ni wito kwetu sisi tupokee urejesho ambao tayari uko kwa Mungu kupitia kwa Kristo. Tunapoukaribisha ukweli wa injili, hatuwezi kufanya lingine bali tunamwambudu mwokozi wetu Yesu Kristo.

SEHEMU YA 2: MASWALI NA MAJIBU:

Basi sasa tushughulikie maswali ya kawaidi na upinzani unaoimbuka kutokana na maelezo ya thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu.

Swali: Unataka kumaanisha hakuna tofauti kati ya mtu ambaye ni Mkristo na mtu ambaye si Mkristo?

Jibu: La hasa. Tunachosema, kwa kuzingatia Yesu ni nani na kutokana na tendo la Kristo kwa wanadamu – waumini na wasioamini – tumeunagishwa upya na Mungu kupitia na kwa Yesu Kristo. Kwa ajili hiyo, wanadamu wote wamerejeshwa kwa Mungu; wote wamekubatiwa kama watoto wapendwa wa Mungu. Wote ndani ya na kupitia kwa Yesu, wameshirikishwa katika ushirika wa upendo na maisha ya Mungu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Licha ya hayo, sio wote wanaojua Yesu ni nani na kwa hali hiyo hawajui wao ni nani katika Kristo. Hivyo sio waumini.

Njia rahisi ya kueleza tofauti kati ya muumini na asiyemuumini ni kwamba wanadamu wote wamerejeshwa (Kwa ujumla) lakini waumini ndio tu wanaoshiriki (binafsi) katika shirikisho hilo.

Tofauti hii inaelezwa mara kwa mara katika agano jipya, na ni ya muhimu sana. Lakini tunatakiwa tusiipeleke tofauti hii mbali na tukafikiria wasioamini hawakumbaliki na Mungu na pia Mungu hawapendi. Tukichukua mtazamo huu, tunakuwa tunasahau ukweli wa Yesu ni nani, na tendo ambalo ameshatekeleza tayari kwa ajili ya kila mwanadamu. Itakuwa tunabadilisha habari njema kuwa habari mbaya.

Tunapowaona wanadamu wote ndani ya Kristo, makundi tuliyokuwa tumejijengea katika mawazo yetu yanasabaratika. Hatuwaoni wasioamini kama watu wa nje mbali tunawaona kama wana wa Mungu wanaohitaji kuelewa ni jinsi gani Mungu anawapenda. Tunawaendea kama ndugu na dada. Je wanajua Kristo ni nani kwao? La! Basi ni nafasi yetu kuwajulisha jinsi Mungu anavyowapenda.

Swali: Kama kweli wote wamerejeshwa kwa Mungu kupitia kwa Kristo, kwa nini maandiko yanaongelea sana kuhusu kutubu na imani?

Jibu: Katika agano jipya, neno la kingiriki lililotafsiriwa “Kutubu” ni “metonia”, ambalo maana yake ni kubadili mawazo. Wanadamu wote wamealikwa na kuwezesha na Roho Matakatifu wabadili mtazamo wao na maisha yao ya dhambi, kujipenda na waelekeze macho yao kwa Mungu na upendo wake wanaoupata kwa maisha yao ndani ya Yesu Kristo kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Tazama wito wa Mtume Petro kwa waumini kubadili mawazo katika Matendo ya Mitume 2:38-39: “Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoloeo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

Mungu huwa halipwi msamaha wake na wanadamu kwa kutubu kwao na kwa imani yao. Kama maandiko yanayosema, msamaha ni zawadi inayotolewa bure kwa neema. Msamaha unakuwepo hata kabla hatujaingia na kuukumbatia.

Ukweli wa injili - ukweli kuhusu Yesu na wanadamu wote kushiriki na Mungu ndani ya Yesu – ni kuwa Mungu tayari ameshawasamehe wanadamu wote kwa msamaha ambao hauna masharti na kwa hali hiyo msamaha ambao hauna gharama kwetu sisi – imeshalipwa. Kwa hali hiyo Petro anatwalika “tubuni na muamini ukweli huu, mbatizwe kwa Roho Mtakatifu kwa fikra za Kristo – ambayo inahusu hakikisho la kiungu kwamba sisi kweli ni wana wa Mungu.

Kutubu ni badiliko la fikra, inahusu kujua Yesu yuko upande wetu na sisi tuko ndani yake, sio kwa jambo ambalo tumelifanya au ambalo tutalifanya. Kupitia kutubu, ambako bado ni zawadi ya Mungu kwetu mawazo yetu yanafanywa upya ndani ya Yesu kupitia kwa Roho Mtakatifu, na tunageukia kwake na kuanza kumwamini.

Roho Mtakatifu anatumiza kutubu kwa kuwa msamaha wetu umeshatimilizwa ndani ya Yesu, dhambi zetu tayari zimesamehewa na kwa hali hiyo sisi tumefanywa viumbe wapya katika Kristo. Katika kutubu huku, tunageuka kutoka kutengwa ndani yetu Roho Mtakatifu anapombatiza fikra zetu kukumbalika ndani ya Yesu na hakikisho tunalolipata kutokana na umbatizo huo.

Swali: Kwa nini Mtume Paulo anasema kuwa kama Roho Mtakatifu haishi ndani yako, wewe hauna uhusiano na Yesu?

Jibu: Warumi 8:9 inasema, “Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa kristo, huyo si wake.”

Sentensi “Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa kristo, huyo si wake.” Haitakiwa kutazamwa kwa nia ambayo haikuandikwa, na kugeuzwa kama dhibitisho kwamba watu wengine si wa Mungu. Kwa mtazamo wa ujumbe huu, Mtume Paulo anawandikia waumini, hatoi tamko kuhusu wasioamini. Yeye anatoa tahadhari kwa waumini ambao wanakataa kumtii na kufuata maelekezo ya Roho Mtakatifu katika maisha yao. Kwa hali hiyo ndio anaendelea kusema “Mnasema kuwa Roho wa Mungu yu ndani yenu, na huo hakika ndio ukweli lakini maisha yenu yanapaswa kuangaza kudhibitisha uwepo wa

Roho wa Yesu ndani yenu”. Mtume Paulo anaendelea kusema katika fungu la 12: “Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili.” (angalia pia fungu 10-17).

Swali: Kama kweli dunia imepata uerejesho, kwanini Yesu akasema haombe ulimwengu?

Jibu: Katika Yohana 17:9, Yesu alisema: “Mimi nawaombea hao; siuombe ulimwengu; bali hao ulionipa, kwa kuwa hao ni wako.”

Kwa kuwa Yesu katika tukio moja alisema haombe ulimwengu, bali anaombea watume, haimanishi kuwa hakuwahi kuombea ulimwengu. Ni hapo tu ambapo maombi yake yanalenga kuwaombea watume.

Ni vema pia kugundua jinsi Mtume Yohana anavyotumia neno “Dunia” (Kwa kingiriki Kosmos) katika mtitilikio wa injili yake. Kwa wakati mwingine dunia inamaanisha wanadamu wote (Sisi wote tunapendwa na Mungu – angalia Yohana 3:16) na wakati mwingine dunia inamaanisha mifumo ya kidunia ambayo inapinga malengo ya Mungu.

Basi ni dhahiri mawazo ya Yesu katika Yohana 17:9. Kwa kuwa mfumo ule unapinga Mungu, Ombi la Yesu halilishirikishi. Haombe dunia kwa hali iliyopo bali anaombea kundi la watu ambao anawatumia kutangaza upendo wake kwa ulimwengu.

Baadaye katika ombi hili, mawazo ya Yesu yanalejerea dunia. Anaomba kwamba wafuasi wake “wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.” (Yohana 17:21). Kama Yohana 3:16 ilivyosema, “.....Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”

Swali: Kama wote tumepata urejesho, kwa nini Biblia inaongea kuhusu Jehanamu?

Jibu: Maandiko yanaongea kuhusu Jehanamu kwa kuwa jehanamu ndio matokeo ya uasi dhidi ya Mungu. Hii ndiyo maana Yesu alikuja. Mungu anatupatia nafasi ya kuitikia wito na kupokea tendo alilotenda Yesu Kristo kwa niaba yetu. Tumeshirikishwa ndani na Yesu, lakini tunaweza kukataa shirikisho hili. Tumerejeshwa kwa Baba lakini pia tunaweza kukataa urejesho huu.

Pamoja na kukataa kwetu, matendo ya Mungu kwa wanadamu wote katika kurejeshwa kwetu kupitia kwa Yesu Kristo hayafutiki.

Katika kitabu cha taraka ya pekee, mwandishi C.S. Lewis aliandika:

Mwishowe wapo watu aina mbili; wale wanaomwambia Mungu “Utakalo lifanyike” na wale Mungu anaowaambia “Utakalo lifanyike” wale wote watakuwa jehanamu wameichagua. Bila uamuzi binafsi hakungekuwepo na jehanamu. Hakuna moyo wenye nia na wenye kutafuta furaha ya Mungu utakosa. Watafutao watapata, wabishao watafunguliwa.

Swali: Kwa nini Biblia inaongea kuhusu watu ambao majina yao hayako kwenye kitabu cha uzima?

Jibu: Ufunuo 13:8 inasema, “Na watu wote wakaao juu ya nchiwatamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.”

Ufunuo 17:8 inasema, “Yule mnyama aliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo Yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako.”

Tunatakiwa kuzingatia mfumo wa uandishi anaoutumia Mtume Yohana wakati akiandika kitabu cha Ufunuo. Mfumo anaoutumia ni kama anafunuliwa, maandiko yake yamejaa ishara. Mfumo huu wa uandishi ulikuwa unatumika sana wakati wa wayahudi na ndio wakati Mtume Yohana alioishi. Hakuna kitabu unaweza kukishika kinachoitwa kitabu cha uzima. Kitabu cha uzima kwa lugha ya uandishi inayoashilia watu wenye uhusiano na Mwana Kondoo. Watu ambao hawako kwenye hicho kitabu inaashilia watu ambao wamekataa maisha mapya ambayo Yesu ameshawadalia na kuwahakikishia.

Swali: Kwa nini Petro anasema ni vigumu kuokolewa?

Jibu: 1Petro 4:17-18 inasema: “Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? Na mwenye haki akiokoka kwa shida, Yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?”

Wazo la msingi katika fungu la 17-18 linapatikana katika fungu la 19: “Basi wao wateswao kwa mapenzi ya Mungu na wamwekee amana roho zao, katika kutenda mema, kama kwa Muumba mwaminifu”

Mtume Petro amekuwa akiwahimiza waumini walikuwa wakiteswa waendeleo kuishi na kutambulika kama wana wa Mungu, na sio kama waasi na wanaoabudu miungu (fungu 1-5).

Kama sehemu ya wamazo yake, anaeleza kwamba mateso ni kama sehemu ya kushiriki katika mateso ya Yesu, na kwa hali hiyo Waumini wanatakiwa kuhimili wanapopitia mateso mbali mbali kwa ajili ya imani na matendo yao, bali wasiwe wanateswa kwa ajili ya dhambi na matendo yasiyo ya Uungu. (Fungu (12-16). Wazo lake ni kuwa waumini wanaotambua kuwa Yesu ni mwokozi na ni hakimu wa haki na wao wote hawatakiwa kuishi katika hali moja na kwa njia moja na wanaompinga Kristo.

Hakika ni vigumu mtu yeyote kuokolewa pasipo Yesu Kristo. Yesu ametenda ambalo lisingewezekana kwa binadamu kujifanyia, lakini kwa wale wanaokataa kushiriki katika mateso ya Yesu; watahiriki katika mateso yao watakapovuna kile wamepanda.

Swali: Ina maana gani hukumu isiyo kikomo na uharibifu wa milele?

Jibu: Danieli 12:2 inasema, “Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele”

2 Wathesalonike 1:6-9 inasema, “Kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi; na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao walioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;”

Mafungu haya mawili yanarejelea wakati wa hukumu kuu atakapofunuliwa Bwana Yesu. (wakati mwingine inasema kurudi mara ya pili kwa Yesu Kristo katika utukufu). Wakati huu ndio wanadamu watakapo oona bayana Yesu ni nani na ni nani wamekuwa na ushirika naye. Na ufunuo huu utawapa nafasi – watasema ndio kwa ushirika na Yesu au la kwa ushirika na Yesu.

Uamuzi wao hautajenga au kuharibu ushirika huo bali utaamua mawazo yao kuhusu ushirika – ama watakumbali upendo wa Mungu kwao na kuingia furaha ya Bwana, au waendeleo kuishi katika kutenganishwa na kudharauliwa (na ndio maana ya dharau na hukumu ya milele na uharibifu). Uharibifu huo ni kujiharibu wenyewe kwa kukataa kuchukua umbo tuliobwa, urejesho tuliopewa tayari.

Katika hukumu kila mmoja wetu atamwona Yesu, ambaye ni hakimu aliyefia kila mmoja wetu, wote tutaamua kama tutamwamini. Watakaomwamini watahiriki katika furaha ya

maisha ya Mungu tuliyopewa katika Kristo. Watakao kataa wataendelea kuishi maisha ya uchungu na jehanamu ambapo wanapaswa.

Swali: Na je ina maana gani “mlango mwembamba”?

Jibu: Yesu alisema katika Mathayo 7:13-14: “Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.”

Yesu anaongea kuhusu maisha tunayoyaishi kwa sasa – upande huu wa ufufuko wa kawaida. Wakati tuliopo wengi wanapita barabara iliyopana ielekeayo upotevuni. Pamoja na kwamba wameshirikishwa ndani ya Yesu, wanaishi kana kwamba hawajashirikishwa. Kwa sasa ni wachache waliokumbatia ukweli yaani Yesu- na yeye ndiye njia nyembamba.

Yesu anaongelea jambo linalofanana na hilo katika Mathayo 7: 21-23: “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”

Hawa watu wametenda miujiza na kwa kuitenda wamepotosha wengi. Wanadai kumjua Yesu, na pamoja na kwamba Yesu anawajua, (yuko kila mahali) hajioni ndani yao hasa akitazama swala la imani, tabia na mienendo na kwa hiyo anatangaza “Sikuwahi kuwajua.”

Swali: Na situnakuwa wana wa Mungu wakati tunapomwamini?

Jibu: Yohana 1:12-13 inasema, “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi wa mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.”

Tumshaona katika maandiko kwamba Mungu ameshirikisha kila mtu katika utu wa kushangaza wa Kristo. Alipokufa, wote tulikufa, alipofufuka wote tulifufuka, wote tulizaliwa upya ndani yake. Kwa hali hiyo wanadamu wote kwa mtazamo wa Mungu ni wanawe. Anawapa wanadamu hiyo “Haki” hata kabla hawajaikumbali.

Wale wanaomwamini na kumkumbali Yesu Kristo wanaingia na kuanza ushirika maisha mapya ambayo yalikuwa yao hata wakati walikuwa hawajamkumbali, maisha ambayo “yamefichwa kwa Yesu ndani ya Mungu.” (Wakolosai 3:3). Kwa kifupi maisha yalivyokuwa

yao kwa ujumla wakati wote huo, sasa yanakuwa yao binafsi na wanaanza kushiriki wanapokuwa waumini.

Swali: Je hii ina maana wote wamejumuishwa?

Jibu: Si kweli kwamba wote wataokolewa hata kama hawakumwamini Yesu. Hakuna wokovu nje ya Yesu Kristo (Matendo ya Mitume 4:12). Lakini kafara ya Yesu inahusisha kila mwanadamu (Warumi 5:8)

Maandiko yanaonyesha dhahiri kuwa Mungu, ndani ya Kristo, amewarejesha wanadamu wote kwake (Wakolosai 1:20), lakini hatamshurutisha mtu yeyote kukumbatia urejesho huo. Upendo haushurutishi.

Mungu anawapenda ndugu na dada wanaompenda kwa furaha ya kujua upendo wake, sio vinyago ambavyo havina akili wala maamuzi yao wenyewe. Kama ilivyofunuliwa kwa Yesu Kristo, Mungu ni upendo kutoka ndani yake, na katika Mungu wa nafsi tatu za Uungu wanavyohusiano mmoja na mwingine kwa pendo la kweli.

Kutazamia kwamba wanadamu wote wataamrejelea Mungu sio ujumuisho wa kila mtu katika wokovu, bali ni kuwa na moyo wenye makusudi ya Mungu (1 Timotheo 2:3-6; 2 Petro 2:3-6; 2 Petro 3:9). Lakini, hatuwezi kujigamba kuwa tunajua kama mwishowe kila mtu atakumbali imani.

Swali: Kama tayari tumeshirikishwa, kwanini kuhangaika kuishi maisha wa Kikristo?

Jibu: Watu wengi hawapendi wazo kwamba watu wengine ambao hawana bidii na kazi ya Mungu kama walivyo wao wataishia kupokea dhawabu kama wao watakoipokea. (Tazama fumbo la waja kazi katika shamba la mizabibu, Mathayo 20:12-15). Lakini wasi wasi huo unamfanya mtu akose kuangalia ukweli kwamba, hata ukifanya kwa kujituma kiasi gani, bado haukustahili wokovu. Ndio maana kwa kila binadamu ni zawadi tusiostahili.

Pamoja na hayo, bado kwenye maandiko tumejifunza kuwa tunaposhiriki sasa ndani ya Kristo, upendo na maisha unazaa matunda mazuri yanayotupa furaha sasa hata milele. Kuishi maishi ya uasi matokeo yake ni uchungu, majuto na lawama kwa mtu binafsi na kwa wengine. Ndio maana Mungu hapendi tuishi maisha ya namna hiyo. Tafakari mafungu yafuatayo:

1 Wakorintho 3:11-15: “Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuweka, yaani, Yesu Kristo. Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi,

kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. Kazi ya mtu aliyoienga juu yake ikikaa, atapata thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto.

Wagalatia 6:7-8: “Msindanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.”

Swali: Je habari gani kuhusu Uinjilisti? Kama kila mtu ameshirikishwa katika upendo wa Mungu kupitia kwa Maisha ya Yesu Kristo, kwa nini tunaitangaza injili kwa ulimwengu na kuwafanya watu wafuasi wa Yesu?

Jibu: Ni ushirika wa Yesu pamoja nasi unayoyapatia maana maisha yetu na kutupa msingi kwa kila nyanja ya maisha yetu, hii ni pamoja na kushiriki katika kazi yake Yesu Kristo. Upendo wa Yesu unatupatia msukumo kushiriki katika mambo anayoyatenda Yesu ulimwenguni kupitia kwa Roho Mtakatifu. Tunaitangaza injili na kuwaalika watu wote kuipokea na kuikumbatia. Kwa kutenda hayo, tunakusudia wajue lililo kweli kwao tayari (kwa hali ya jumla) litadhihirika kwao kama kiumbe (kwa hali ya binafsi).

Swali: Tunaweza kulieleza je andiko la Yohana 6:44?

Jibu: Yohana 6:44 inasema, “hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho.”

Viongozi wa kidini wa kiyahudi walikuwa wanatafuta njia za kutoa Yesu kwenye lengo. Kwanza walikuwa wameghadhabishwa na msemu kuwa “Mimi ni chakula kitokacho mbinguni” (Yohana 6:41). Tamko hili likionekana kwao kama lililokusudiwa kujifananisha na Mungu.

Majibu ya Yesu kwa malalamiko yao kuhusu tamko hili lilikuwa waache kunung'unika (fungu 43) na kwa kuzingatia kuwa “hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka... (Fungu 44) kwa kifupi Yesu ana maana kuwa wanadamu hawataitikia wito pasipo Mungu kuwawezesha kuuitikia wito.

Katika fungu hili, Yesu hachuji idadi ya watu watakaovutwa kwake bali inadhihirisha kuwa anafanya kazi ya Baba. Katika sehemu nyingine anasema “nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.” (Yohana 12:32) na kwa kuwa Yesu anafanya yale Mungu amekusudia ayatende, Yohana 12:32 inaonyesha kuwa Baba hakika anawavuta watu kwa Yesu.

Swali: Kama kweli ulimwengu wote umeshirikishwa kwa Yesu, kwanini basi dunia imejaa maovu?

Jibu: Ufalme wa Mungu hautadhihirika mpaka atakaporejea Mwanaye Yesu Kristo. Kama Petro alivyohubiri siku ya Pentekoste, “Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. Matendo ya Mitume (3:19-21)

Kwa sasa, tunapata hakikisho katika maneno ya Yesu: “Hayo nimewambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwengu mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu” (Yohana 16:33)

Swali: Unailinganishaje thiolojia hii ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu na ile ya Calvinism na ya Arminianism?

Jibu: Katika kuzilinganisha thiolojia hizi tatu za Kikristo, tunaongea kuhusu mitazamo ya ndugu na dada wenye nia moja ambayo ni kumtumikia Kristo. Kwa hali hiyo mjadala wetu unapaswa kuonyesha heshima na utulifu sio malingo na chuki dhidi ya wengine.

Calvinism ni thiolojia ambayo ilibuniwa kutokana na mafunzo ya mwalimu wa kiprotestanti ya John Calvin (1509-1564). Calvinism inasisitiza nguvu za Mungu kuinua na kutoa wokovu kwa wanadamu. Wanaoufuata mfumo huu wa thiolojia wanaeleza kuwa wapo waumini wa Mungu ambao ni “wateule” wa Mungu, hawa wateule ni kundi ambalo limetengwa na ulimwengu; na ndio wale Yesu alifia msalabani. (neema kwa wachache). Hao wateule kazi ya wokovu wao ilifanyika hata kabla ya kutambua kwao na kuukumbali wokovu wao. Kulingana na thiolojia ya Calvinism, hao wateuli waliofiwa na Yesu hawawezi kuuepuka wokovu na kwa njia moja au nyingine lazima wataukumbali wito. “Neema ambayo haiepukiki.”

Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ina tofautiana na hii ya Calvinism katika upana wa urejesho. Biblia inaeleza bayana kuwa Kristo alifanya upatanisho sio tu kwa dhambi zetu bali kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:2). Na wakati thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ikitofautiana na thiolojia ya Calvinism, kuhusu upatanisho wa wachache, na urejesho wa wateule peke yao, inakumbaliana na Calvinism kuhusu msamaha wa dhambi, urejesho, ukombozi na kufanywa haki kwa wanadamu na Mungu, haya yote yalitimizwa kwa pamoja na tendo la Kristo msalabani, ukweli huu hauzingatii tunayoyafanya au tusiyoyafanya.

Thiolojia ya Arminianism ilibuniwa kutokana na mafunzo ya mwalimu kiprotestanti ya Jacob Arminius (1560-1609). Arminius alisisitiza kuwa Yesu alifia wanadamu wote, na

kwamba watu wote wanaweza kuokolewa endapo wanaweza kuchukua hatua zinazopaswa, matendo ya binafsi ambayo yatawezesha na Roho Mtakatifu. Thiolojia hii bila kupuzilia ukuu wa Mungu huegemea maamuzi ya binadamu na kujiamulia kwao. Misingi yake mikuu ni kuwa wokovu, msamaha wa dhambi, upatanisho, ukombozi, kuhesabiwa haki, hazifanyiki kikamilifu bila kuwa na imani.

Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu ina tofautiana na hii ya Arminianism hasa kuhusu nguvu ya urejesho. Upatanisho, kati ya Mungu na wanadamu ni kama kitu kilicho juu sana kwa wanaoifuata thiolojia ya Arminians; upatanisho kwao hauwezi kuwa imara au dhambiti pasipo maamuzi ya imani kwa mwanadamu. Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu kwa upande mwingine inafundisha kuwa upatanisho na urejesho ni hakika kwa wanadamu kwa ujumla hata kabla ya wao kuitikia na kuukumbali kibinafsi.

Pamoja na kwamba thiolojia za Calvinism na Arminianism zote mbili zinasisitiza mifumo miwili tofauti ya thiolojia, Thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu imejaribu kama Church Fathers Irenaeus, Athanasius, na Gregory zilivyofanya kuzingatia mtiririko wa upana unaozingatiwa na Armanians na mkazo unaowekwa na wana calvanism.

Swali: Je perichoresis ni nini?

Jibu: Muungano wa kiundani wa upendo ambao Baba, Mwana na Roho wanaoshiriki katika ushirika wa nafsi tatu za Uungu, ni muungano wenye mshikamano wa kushangaza, muungano unaowawezesha mmoja kuishi ndani ya mwingine bila kupoteza ubinafsi wake. Kama Yesu alivyosema: “..... Mpate kujua na kufahamu wa kuwa Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba” (Yohana 10:38). Mwanathiolojia mwenye asili ya Kingiriki alieleza uhusiano huu kwa kutumia neno perichoresis ikiwa na maana pamoja na, na ndani ya. Kila nafsi katika ushirika yuko ndani ya mwingine na anaishi pamoja na mwingine.

Mwongozo wa mitazamo ya Biblia:

Katika kitabu hiki, tunajaribu kushughulikia maswali na upinzani unaoimbuka dhidi ya mfumo wa thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu. Bila shaka yapo mafungu mengine ambayo yataimbua maswali na upinzani dhidi ya hii thiolojia. Lakini tulilojaribu kufanya ni kuiwakilisha thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu, Yesu kama kiini ili iwe mtazamo na mwongozo wetu tunaposoma Biblia.

Wengine wanapinga wazo la kutafsiri Biblia. Huwa wanasema “Huwa naiachia Biblia iseme vile inasema”. Wazo hili japo linavutia, sio la kuzingatwa kama la kweli. Tendo la kusoma linaenda pamoja na kutafsiri. Kwa hiyo sio swala la kutafsiri bali ni tunatumia mfumo gani wa thiolojia kutafsiri tunapoisoma Biblia?

Wakati mwingine huwa tunasoma Biblia tukiwa na mitazamo na misimamo ya awali. Tunachosisitiza hapa ni kuwa ukweli wa Yesu Kristo ni nani ndio uwe mwongozo wetu tunaposoma na kutafsiri Biblia. Yesu Kristo lazima awe ndarubini tunayotumia kusoma maandiko.

Kwa hali hiyo, tunaposoma maandiko, tunapendekeza kujiuliza maswali yafuatayo:

- Fungu hili lina uiano gani na injili? Ambalo linajibu swali “Yesu ni nani?”
- Fungu hili linarejelea wokovu wa wanadamu wa ujumla, wokovu wa mwanadamu binafsi na ushirika wake na Yesu au kuukataa wokovu kwa mwanadamu?
- Je ni nini historia, utamaduni wa wanaoongelea kwenye fungu hili?
- Fungu hili kwenye tafsiri zingine za Biblia linasomekaje? Hakika tafsiri zingine zinaweza kusaidia kuona fungu kwa mtazamo mwingine. Pia inasaidia kuangalia ufafanuzi wa Kingiriki na tafsiri zingine kwa sababu maana ya fungu inaweza kupotea wakati likitafsiriwa kutoka kwa lugha ya kingiriki.
- Kwa muongozo wa mifumo ya kusoma Biblia unaweza kusoma vitabu vifuatavyo: *How to Read the Bible for All Its Worth*, na Gordon D. Fee na Douglas Stuart (Zondervan, 1981, 1993) au *Elements of Biblical Exegesis: A Basic Guide for Students and Ministers*, by Michael J. Gorman (Hendrickson, 2009).

Maelezo ya msingi yatokanayo na thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu, kiini chake akiwa Yesu Kristo.

Ifuatayo ni miongozo ya msingi wa thiolojia kama ilivyoielezwa kwenye kitabu hiki.

1. Mungu katika nafsi tatu za Uungu aliumba mwanadamu ili ashiriki upendo wanaoshiriki Baba, Mwana na Roho Mtakatifu kupitia kwa nafsi ya Yesu Kristo aliyefanywa mwanadamu kwa njia ya kushangaza.
2. Mwana akabadilika na kuwa mwanadamu, Yesu Kristo, kwa nia ya kuleta urejesho wa wanadamu wote kwa Baba kupitia kwa kuzaliwa, maisha, kifo, ufufuo na kupandishwa.
3. Yesu Kristo aliye sulubishwa ndiye mwakilishi wa wanadamu katika mkono wa kuume wa Baba na anavuta wanadamu wote kwake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
4. Ndani ya Yesu, wanadamu wanapendwa na kukumbaliwa na Baba.
5. Yesu Kristo, alilipa deni letu lote la dhambi – la nyuma, la sasa na la usoni – na hakuna deni limesalia kulipwa.
6. Baba katika Yesu, ametusamehe dhambi zetu zote, na wanatazamia ukumbali wetu wa msamaha huo na kumrejelea.

7. Tunaweza tu kufurahia upendo huu tutakapo amini kwamba anatupenda. Tunaweza kufurahia msamaha wa dhambi tutakapo amini kwamba ametusamehe.
8. Tunaitikia wito wa Roho kwa kurejelea Mungu, kwa kuamini habari njema, kuubeba mslaba wetu na kumfuata Yesu, Roho anatuongoza kuishi maisha yanayokubalika ndani ya ufalme wa Mungu.

Text Found at the Grace Communion International Website:

<http://www.gci.org/>

Translated from English to Kiswahili by:

Francis Wanyoike – GCI Kenya

Email: nyoikefg@gmail.com